

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI



Simu: +255 754 034 858

Barua Pepe: karangass2016@gmail.com

Kumb. Na. KSS/JI/2020/_____

Karanga Sekondari

S.L. P 8747

Moshi.

Tarehe: 15.12.2020

Jina la mwanafunzi:

.....

S. L. P

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KARANGA

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020. Shule ya Sekondari Karanga ipo umbali wa km 2 magharibi mwa mji wa Moshi kutokea barabara kuu ya Moshi – Arusha na kutokea lango kuu la Gereza la Karanga.

Usafiri wa boda boda (pikipiki) ni Tshs. 1,500/= au kutembea kwa miguu. Kutokea Moshi mjini unapanda daladala (Hiace) za Soweto – Shirimatunda kwa nauli Tsh. 400/= hadi mwisho wa gari kisha unatembea mwendo mfupi kwa kuulizia ilipo shule. Shule itafunguliwa tarehe 06/01/2020 saa moja kamili asubuhi.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

- Sare ya shule hii utakayopaswa kuvaa ni suruali (2) kwa wavulana na sketi (2) kwa wasichana (rangi ya kitambaa cha suruali / sketi imeambatishwa na fomu hii) kwa wote na mashati mawili (2) meupe kwa wote. Tafuta kitambaa chenye ubora wa juu zaidi ya hicho cha mfano.
- Hijabu nyeupe ya kushona inayoishia kwenye mabega kwa wasichana wa kiislamu.
- Uwe na nguo za kimichezo (jozi mbili) ya rangi bluu au nyekundu.

NB: Kwa wasichana sketi ziwe za marinda box mbele na nyuma na wavulana suruali iwe na marinda mawili pande zote na iwe na turn up chini.

2.2 Daftari (12 Counter Book Q₂ au Q₃), kalamu, penseli, rula, daftari ndogo ya mazoezi kwa kila somo kwa ajili ya majaribio ya kila wiki, Mathematical 4 figures na mkebe wa hesabu.

2.3 Karatasi nyeupe Rimu 1 uje nayo siku ya kupokelewa shuleni.

2.4 Gharama ya chakula cha mchana ni 100,000/= kwa mwaka au 50,000/= kwa muhula na ilipwe kabla au siku ya kufungua shule kwenye **NMB: Karanga Secondary School Project Account 40310025024** na ulete **Bank Pay in Slip** siku ya kufungua shule.

3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyoboreshwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye

jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti: -

- 1) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- 2) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- 3) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- 4) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- 5) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- 6) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- 7) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- 8) Kutunza mali za umma.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule: -


- 1) Wizi;
- 2) Uasherati na ushoga;
- 3) Ubakaji;
- 4) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- 5) Makosa ya Jinai.
- 6) Kupigana au kupiga.
- 7) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- 8) Kudharau Bendera ya Taifa.
- 9) Kuoia au kuolewa.
- 10) Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
- 11) Kutoa mimba.
- 12) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- 13) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- 14) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mwanafunzi anayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni: -

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KARANGA



Mkuu wa Shule

**THE HEADMASTER
KARANGA SEC. SCHOOL
P.O. BOX 8747, MOSHI**